



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. **MDC/ADM/10/30/VOL. I/90**

17/04/2023

### **YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imepata idhini ya kutekeleza Ikama na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kupitia barua **Kumb. Na.FA.97/228/01"TEMP"/06** ya tarehe **06 Aprili, 2023** iliyotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Maswa anatangaza nafasi za kazi ya **Mtendaji Daraja la III** kwa Masharti ya kudumu, Hivyo Watanzania wote wenye sifa hizo mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo:-

#### **1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI - [10]**

##### **1.1. Sifa za Mwombaji:-**

- Wahitimu wa kidato cha nne au sita wenye cheti cha [NTA Level 5] au Certificate katika moja ya fani zifuatazo.
- Utawala
- Usimamizi wa Rasilimali watu
- Maendeleo ya Jamii au
- Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
- Usimamizi wa fedha [Local Government Accounting and Finance]
- Astashahada ya Sheria
- Awe na umri usiozidi miaka 45
- Awe na cheti cha kuzaliwa.

## **1.2. MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji,
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafasiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- xiii. Kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri.

## **1.3 NGAZI YA MSHAHARA**

**Mshahara:** Ngazi ya TGS B kwa mwezi.

## **2.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI II – NAFASI - [02]**

### **2.1. Sifa za Kitaaluma kwa Mwombaji:-**

- Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV waliohudhuria Mafunzo ya Uhaziri na kufaulu mtihani wa Hatua ya Pili (Diploma). Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na kiingereza maneno 100 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya komputa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali katika Programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-Mail na Publisher na kupata cheti.

## **2.2. MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka mbalimbali.
- ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kupokea majalada, kuyagawa na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

- iv. Kutafuta na kumpatia Mkuu wake Majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi.
- v. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Mwajiri au Msimamizi wake wa kazi.

## 2.3 NGAZI YA MSHAHARA

**Mshahara:** Ngazi ya TGS C kwa mwezi.

## 3.0. MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji waambatanishe na nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na Wakili au Mahakama.
- Muombaji ambatanishe picha mbili [2] ndogo ya rangi [passport size] ya hivi karibuni
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita [form VI and form IV result slip] **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

## 4.0. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,  
S.L.P. 170,  
**MASWA –SIMIYU.**

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 30/04/2023 Saa 9.30 Alasiri.**



Simon Berege  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
MASWA**